CS1858

# *Ujumbe Kwa Kanisa la Efeso*

### *Mstari wa 4*

### Kuupungua Kwa Upendo wa Kwanza

" Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza." **Ufunuo 2:4** .

NI JAMBO KUBWA SANA kusema mengi katika pongezi zetu kama ilivyosemwa kuhusu kanisa la huko Efeso. Soma haya "Yesu Kristo, ambaye ndiye shahidi mwaminifu," alisema juu yao " Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo; tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya jina langu, wala hukuchoka." Lo, ndugu na dada zangu wapendwa, tunaweza kuhisi kushukuru kwa dhati ikiwa tuna unyenyekevu, lakini kwa kusema ukweli, kwamba pongezi hili linatumika kwetu. Heri mtu ambaye kazi zake zinajulikana na kukubalika kwa Kristo. Yeye sio Mkristo mvivu, ana utauwa wa matendo; anatafuta kazi za utauwa kama kutii sheria nzima ya Mungu, kwa kazi za hisani kuonyesha upendo wake kwa undugu, na kwa kazi za kujitolea kuonyesha kiambatisho chake kwa sababu ya Mwalimu wake. "Ninajua kazi zako." Ole! wengine wako hawawezi kufika mbali kisasi hicho. Yesu Kristo mwenyewe hawezi kushuhudia kazi zako, kwa kuwa haujafanya chochote. Wewe ni Mkristo kwa taaluma, lakini wewe sio Mkristo kwa matendo yako. Ninasema tena, ni furaha kwa yule mtu ambaye Kristo anaweza kumwambia, "Ninajua kazi zako." Ni pongezi inayofaa kwa ulimwengu kuwa na mengi kama hayo yaliyosemwa juu yetu. Lakini zaidi, Kristo alisema, "na kazi yako." Hii bado ni zaidi. Wakristo wengi wana kazi, lakini ni Wakristo wachache tu wanaotekeleza kazi zao.

Alikuwa "akifanya kazi nyingi zaidi." Wengi walikuwa katika siku za mtume ambao walifanya kazi kwa Kristo; lakini kabla ya hapo, Mtume Paulo alifanya kazi kwa roho. Sio kazi tu, ni kazi ya wasiwasi; inatoa nguvu yote, na kutumia nguvu zote kwa Kristo.

Je! Bwana Yesu anaweza kukuambia "Najua kazi yako?" Hapana. Anaweza kusema, "Ninajua chukizo lako; Ninajua uvivu wako; Ninajua ulegevu wako wa kazi; Najua kujivunia kwako kile unachofanya; Najua nia yako ya kufikiria kitu, wakati wewe sio chochote." Lakini ah! marafiki, ni zaidi ya wengi wetu tunathubutu kutumaini kuwa Kristo anaweza kusema, "Ninajua kazi yako."

Katika nafasi ya kwanza, upendo wetu wa kwanza ulikuwa nini? Pili, tulipotezaje? Na tatu, wacha nikuhimize upate kuelewa tena.

Sasa ni upendo wa kwanza kwamba wewe na mimi lazima nikiri kwamba ninaogopa tumepotea kwa kipimo. Wacha tuone ikiwa tunayo hayo. Wakati tulipenda Mwokozi kwa upendo wa kwanza jinsi tulivyokuwa na bidii; hakukuwa na kitu kimoja katika Biblia, kwamba hatukufikiria thamani zaidi; hakukuwa na amri moja yake hatukufikiria kuwa kama dhahabu nzuri na fedha za kuchaguliwa. Milango ya nyumba yake hukuwai kufunguliwa bila kuwa huko. ikiwa

kulikuwa na mkutano wa maombi saa yoyote katika siku ambayo tulikuwa huko. Wengine walisema juu yetu kwamba hatuna uvumilivu, tungefanya sana na kufunua miili yetu mara nyingi lakini hatukuwahi kufikiria kwamba "Usifanye mwenyewe," ilizungumzwa masikioni mwetu; lakini tungefanya chochote wakati huo. Kwa nini wapo wengine  ambao hawawezi kutembea kwenye Ukumbi wa Muziki asubuhi,ilhali wanatembea mbali sana. Wakati wa kwanza kujiunga na kanisa, ungetembea mara mbili hadi sasa. Kuna wengine  ambao hawawezi kuwa katika hadhara ya mkutano wa maombi,hawakubali; lakini wakati ulibatizwa kwanza, hakukuwa na mkutano wa maombi ambao ulikosa kuhudhuria. Ni upotezaji wa upendo wako wa kwanza ambao unakufanya utafute faraja ya miili yako badala ya ustawi wa roho zako.

Upendo huo wa kwanza haudumu muda mrefu kama tunavyohitaji. Wengine wengi  hutafuta sababu hata hapa; hauna upendo huo wa kuwasha, upendo huo unaowaka, upendo huo wa ujinga kama ulimwengu ungeiita, ambayo ni baada ya upendo wote kutamaniwa na kudhaminiwa. Hapana, umepoteza upendo wako wa kwanza kwa heshima hiyo.

Tena, jinsi ulivyokuwa mtiifu. Ikiwa uliona amri, hiyo ilikuwa ya kutosha kwako kufanya. Lakini sasa unaona amri, na unaona faida upande mwingine; na mara ngapi unashirikiana na faida na uchague majaribu, badala ya kutoa utii usio na kipimo kwa Kristo.

Pia:tulipokuwa katika upendo wetu wa kwanza,tungemfanyia Kristo nini; basi twawezaje kufanya machache.Baadhi ya matendo tuliyoyatenda wakati tulikuwa wachanga katika Ukristo,japo tulikuwa ndiyo tumebadilika,tuliangalia nyuma  matendo hayo,yalikuwa mambo makubwa na sio hadhithi ya abunuasi.Unakumbuka wakati ulikuwa kijana na ukamjia Kristo,ulikuwa na kitu muhimu kwa mfuko wako;kilikuwa ni peke yake ulicho nacho kwa mfuko wako,na ukakutana na mtakatifu maskini na ukampa chote.Haukujuta kwamba umempa,majuto yako yalikuwa ni kwamba ungekuwa na kiasi kikubwa cha kumpa basi ungempa.Ulikumbuka kwamba kitu kilihitajika kwa ajili ya Kristo.Hakika tungetoa chochote wakati ule tulianza kumpenda Mwokozi.Ikiwa kulikuwa na mahubiri ambayo ungefanyika maili tano,basi tungemsindikiza mhubiri ili tumfariji katika giza,tulikuwa chonjo.Ikiwa kulikuwa na shule ya Jumapili,hata kama ilikuwa asubuhi na mapema,tungerauka,ili tuwe mahali pale.Matendo makubwa yasiyosikika,ni baadhi ya mambo ambayo tukiyaangalia kwa mshangao,tungeyafanya.Kwa nini hatuwezi kuyafanya sasa hivi?

Je,wajua kwamba kuna watu ambao mara nyingi huishi jinsi walivyokuwa.Nanena waziwazi sasa.Najua kuna ndugu katika kanisa hili ambaye anaweza kukwazika.Natumai atakwazika.Siyo miaka mingi iliyopita nikimwuliza kwa nini hajafanya kitu. “ Ndiyo,nimetekeleza jukumu langu,nimekuwa nikifanya hivyo,na nimefanya pia mengine;nimefanya hiki na kile.” Mungu amwuokoe,na hata sisi sote kwa kuishi kwa dhana kwamba tumekuwa “tukifanya hivi” Hakuna kitu kitafanyika ikiwa tunasema kwamba tushafanya.Itakuwaje dunia ikisema kwamba “nimezunguka sana,kwa hiyo inatakikana nisimame wima”. Wacha bahari iseme,nimekuwa nikipwa na kububujika kwa miaka hii mingi,kwa hivyo sitapwa na kububujika tena.” Wacha jua liseme, “Nimekuwa nikichomoka na kutwaa kwa siku nyingi sana;nimefanya hivi kiasi cha kunipa jina jema;sasa nitasimama”; na wacha mbalamwezi pia ujifunike na giza na kusema, “ nimekuwa nikiangaza sana usiku mwingi na nimekuwa nikimwangazia msafiri na mkaaji wa Maroko.Nitazima mwanga wangu milele na kuwa na giza milele.” Wapendwa ikiwa mmoja wetu atawacha kufanya kazi basi tukose kuishi.Mungu hana kusudi la kutuacha tuishi maisha yasiyo

na maana.Lakini ujue kwamba,tukiacha kazi zetu za kwanza,hakuna suala kwamba hatujaacha upendo wetu wa kwanza;hio ni hakika.Ikiwa kuna nguvu inayobaki,ikiwa kuna uwezo wa kiakili na kimwili,tukiacha afisi yetu,tukiacha kazi zetu,hamna suluhisho la suala hili ambalo dhamiri zetu itakubali,ila tu hili; " Umeacha upendo wako wa kwanza,kwa hivyo umepuuzia kazi yako ya kwanza." Ndiyo! Tulikuwa tayari kutoa sababu ya kuepa kazi.Wahubiri wengi wamestaafu kutoka kwa huduma mapema sana kabla hajawa wa kustaafu.Ameoa mwanamke tajiri.Mtu mwingine amemwachia pesa kiasi,na yuaweza kuendelea bila huduma.Alikuwa ameanza kuwa mnyonge katika njia za Mungu,ama kwa njia nyingine angesema, " Mwili wangu na nguvu zangu nimeziacha,kwa hivyo nimeacha kufanya kazi na kuishi."

Na wacha mtu yeyote ambaye alikuwa mwalimu wa watoto wa Jumapili,ambaye alikuwa akigawanya majarida kisha akaiacha,ambaye alikuwa akifanya bidii katika njia ya Mungu lakini sasa amekuwa mvivu,asimame usiku wa leo kwenye kizimba cha dhamiri yake,na kutetea mashtaka ninayoyaleta dhidi yake,kwamba ameuacha upendo wake wa kwanza.

II.Na sasa,mpendwa,NI WAPI tuliuachia UPENDO WETU WA KWANZA,ikiwa tumeupoteza upendo huo?---

Ndiyo,ulimwengu mwingi ni kitu kibaya kwa mwanadamu yeyote! Ninajiuliza sana ikiwa mtu anapaswa wakati mwingine kuuacha,na kusema, "Kuna nafasi ya kufanya biashara zaidi,lakini itahitaji wakati wangu wote,na inabidi niuache wakati ule wa kuomba,kwa hiyo sitaifanya biashara kabisa;ninayo ya kutosha,kwa hivyo wacha ikae.Afadhali nifanye biashara na mbingu kuliko kufanya biashara na dunia." Lakini sababu nyingine ni hivi.Je,unakumbuka kweli kwamba pengine umesahau unachodaiwa na Kristo? Kuna jambo moja,ambalo nasukumwa kufanya kila wakati kama vile kurudi nyuma mahali nilianzia:

" Mimi,mkuu wa wenye dhambi,Lakini Yesu alinifia."

Mimi na wewe tunaongea juu ya kuwa watakatifu;twajua uchaguzi wetu,twafurahia wito wetu,twaenenda kwa utakaso;na kusahau shimo la taka tulilotolewa.Kwa hivyo ndugu yangu,wewe sio ,mtu yeyote lakini ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema,kumbuka jinsi ungekuwa,ikiwa Mungu angekuacha.Na kwa hakika,kwa kurudi kwa kanuni za kwanza,na kwenye jiwe kuu la msingi,msalaba wa Kristo,basi utaongozwa kurudia upendo wako wa kwanza,Kuna sababu elfu ningependa kutoa,lakini nawaachia kila mtu kuangalia moyo wake,kujua kwa nini kila mmoja wenu ameupoteza upendo wake wa kwanza.Bado kuna jambo fulani,wapendwa wangu wa dhati,tukiupoteza upendo wetu wa kwanza,walimwengu watasemaje kutuhusu ikiwa upendo wetu umetoweka? Naweza nikasema hivi,sio kwa majina yetu lakini kwa ajili ya jina la Mungu.Je,ulimwengu utasemeje kutuhusu? Kulikuwako na wakati,na wakati huo haujapotea bado ambapo watu lazima watazame kanisa hili,na kusema hivi kuhusu kanisa, " Kuna Kanisa,ambalo ni kama oasisi yenye mwanga katikati ya nyikani,kurunzi ya mwangaza kati kati ya giza." Mikutano yetu ya maombi ilikuwa mikutano ya maana,kusanyiko lilikuwa makini wakiwa wengi.Je,unakunywaje maneno;jinsi macho yako yalimeremeta na moto wa uzima,wakati wowote jina la Kristo lilitajwa! Na itakuwaje,kwa muda mfupi utakoposemwa, " Haya,Kanisa lile,linasinzia kama na mengine,hebu waangalie hata wakati mhudumu anapohubiri,wakisinzia na kulala,na hawajali mahubiri.Tazama,wamekuwa baridi kama na kutojali kama na wengine.Walikuwa wakiitwa wapiganaji wakuuu katika ulimwengu,kwa

sababu walikuwa tayari kutetea jina la Bwana wao na ukweli wa Bwana wao,na baadaye wakapata jina hilo kama matokeo,lakini sasa unaweza kuapa mbele yao na hawatakukemea:jinsi walivyokuwa wakiishi kwa Mungu na nyumba yake,walikuwepo pale kila wakati;tazama hata mkutano wao wa maombi,wangejaza viti vyao kamili katika mkutano wa maombi kama huduma ya kawaida;lakini sasa wamerudi nyuma." Ndiyo,nilisema ulimwengu, "kama vile nilivyosema ni ukweli kwamba,ilikuwa tukio la ghafula tu,msisimko mchache tu wa kiroho,na umerudi nyuma." Na ulimwengu wasema, "Kwa hivyo ningekuwa nao,ningekuwa nao!"

Umeonywa, kila mmoja wenu; umeambiwa kwa dhati kujitafuta na kufanya kazi yake fupi. Na ikiwa yeyote kati yenu atakuwa mnafiki, katika siku kuu ya Mungu, mwenye hatia kama ninavyoweza kuwa katika hali nyingi, kuna jambo moja ambalo niko wazi kuwa sijashtuka kutangaza shauri lote la Mungu. Siamini kuwa watu wowote ulimwenguni watahukumiwa sana kuliko vile utakavyoangamia; kwa jambo hili sijashtuka kusema uovu mkubwa wa kutengeneza taaluma bila kuwa na sauti moyoni. Hapana, hata nimeenda karibu sana na utu, hata sikuweza kwenda mbali zaidi bila kutaja majina yako. Na hakikisha, neema ya Mungu kuwa pamoja nami, wala wewe wala mimi mwenyewe hautaokolewa kwenye mimbari katika dhambi yoyote ya kibinafsi ambayo naweza kuona katika yeyote kati yenu. Lakini oh, wacha tuwe waaminifu! Bwana mapema agawanye kanisa hili hadi sehemu ya kumi tu ya wewe ibaki, kuliko hapo awali ili kuzidishwa mara mia isipokuwa umezidishwa na walio hai katika Sayuni, na kwa kundi takatifu ambalo Bwana mwenyewe ameteua, na atashika mwisho. Kesho asubuhi, tutakutana pamoja na kusali, ili tuweze kuwa na upendo wetu wa kwanza kurejeshwa; na natumai wengi wenu mtapatikana hapo kutafuta tena upendo ambao umepotea. "Na wewe ambaye hajawahi kuwa na upendo huo hata kidogo, Bwana anapumua juu yako sasa kwa upendo wa Yesu. Amina….Wacha makapi yatoke,lakini ikiwa ngano inabaki basi tuna faraja.Wacha wale waabuduo walioko nje wakose kusikia,kile kinachomanishwa? Wacha wageuke,lakini ninyi wanajeshi wa Msalaba,ukigeuza mgongo wako katika siku ya vita,ni wapi nitaficha kichwa changu? Ni nini nitasema kuhusu jina la Mwokozi wetu,au mtukufu wa injili yake? Ni fahari na furaha kwamba mafundisho ya kale yamefufuliwa siku hizi na ukweli…jambo Paulo alihubiri,na lile Yesu alihubiri,bado lna nguvu ya kuokoa na linashinda kwa mbali katika nguvu mafundisho ya kichanga na imani potofu ya wakati huu.Lakini wazushi watasema;lakini  nini,wakiyaona mambo haya yote? "Haya," watasema, " kwamba ukweli wa zamani uliohimizwa na ulokole wa kijana mdogo mpumbavu,uliawaamsha watu wachache;lakini ulikosa upako na nguvu,na ukweli huo wote ukazimia!" Je,mtakosa kumheshimu Bwana na Kiongozi wako enyi wana wa Mfalme.Nawasihi msifanye hivyo bali jaribu kupokea tena kama karama yako njema ya Roho ya upendo wa kwanza.Je,kuna watu miongoni mwenu ambao wanakiri dini,lakini hawaishi kulingana na dini? Basi,wacha kazi yako,ama pokea ukweli na usiuze.Nendeni nyumbani kila mmoja,na uangaze macho yako kwa Mungu,na umwombe akuchunguze,na kukujaribu,na kujua njia zako,ilia oane kama kuna njia mbaya ndani yako,na uombe kwamba akulinde kwa njia ya uzima wa milele.Na ikiwa umakiri tu lakini hujamilika ,basi mtafute Bwana japo anapatikana na umwite angali karibu.Umeonywa,kila mmoja wenu;umeambiwa ujipige msasa na urekebishe.Na ikiwa mmoja wenu ni mnafiki,katika siku kuu ya Mungu,hata nikiwa na hatia kwa njia nyingi,kuna jambo moja ninayajua kwamba nimetangaza shauri lote la Mungu.Siamini kwamba watu fulani katika ulimwengu watahukumiwa kuliko wewe ukizimia

### *Mstari wa 4 na 5*

**Kupenda Kulalamika**

" Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu.” (**Ufunuo 2:4-5** ).

ILIKUWA NI kazi ya Kuhani kuenda katika patakatifu na kuwasha taa za dhahabu:tazama jinsi Kuhani wetu Mkuu anatembea kati ya taa za dhahabu saba:kazi yake siyo ya mara kwa mara,lakini ni ya kudumu.Akivaa kanzu ambazo zilikuwa za kifalme na za kuhani,anaonekana akiwasha taa zilizo takatifu,akimimina mafuta matakatifu,na kuutoa uchafu ambao waweza kuuzima taa.Kwa kuwa yeye ni mwangalifu sana,basi yeye ndiye astahiliye sana. Yeye,mara nyingi ndiye “Shahidi mwaminifu na wa kweli.” Anao upendo sana kwa hivyo,hawezi kuhukumu kwa hasira.Ana upendo mwingi,kwa hivyo yuaweza kuhukumu kwa uwivu.

Uwivu ndio uwakilishi wa upendo kama wake.Hawezi kuyaongea maneno laini au maneno makali; walakini atayaongea ukweli,ukweli katika upendo,ukweli kama vile anavyoelewa.Basi ndiyo maana yuasema, “ Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa,” kwa sababu maneno yake ni ya kweli sana,ya haki sana,na yana uzito.Kwa hivyo nahisi kwa wakati huu kwamba twaweza kuungana katika maombi kwa Bwana Yesu ili aje kati kati yetu na aweke nuru yetu kwa utaratibu ipate kuangaza.Kwa kutembelea sisi yeye mwenyewe kama alivyowatembelea makanisa saba ya Asia katika njozi! Kwake yeye kuna mafuta ya kuilisha mwali ulio hai,na anajua jinsi ya kuyamimina mafuta hayo kulingana na kipimo; kwake yeye ana misumaa ya dhahabu ambayo anaweza kutumia kuondoa utukutu nyepesi,ili kwamba nuru yetu iangazie wanadamu,ili kwamba wazione kazi zetu njema,na wamtukuze Baba yetu aliye mbinguni. Kwa uwepo wake sasa,ili atuchunguze na kututakasa, ili kwamba atuweke tung’ae kwa utukufu wa sifa zake Baba! Tutaweza kuhukumiwa na Bwana,ili kwamba tusihukumiwe na ulimwengu.Twaweza kuomba asubuhi hii, “Nichunguze,Mungu,Ee Mungu,na upate kujua haja za moyo wangu: nijaribu,ili ujue fikra zangu; ili uone kama kuna njia potofu ndani yangu,na uniongoze kwenye njia ya uzima.” Haya yote yako wazi na yanaonekana katika macho ya yule ambaye yuataka kufanya kazi; na tunapenda iwe hivyo. Twakukaribishe,Ewe Kuhani Mkuu,ili uje katika Hekalu hii,na uangalie taa hii asubuhi ya leo.

Kwanza kabisa,tunagundua kwamba ANATUELEWA.Lakini hii ndiyo hoja yetu kwa wakati huu,kwamba hata kama Yesu anaweza kuyaona yaliyo mema,*japo kwa uaminifu yuaona yale yaliyo maovu*.Upendo wake sio kipofu.Hasemi, “Kwa wale wote niwapendao nawapongeza;” walakini, “ Kwa wale wote niwapendao,nawakemea na kuwarekebisha.” Ni vizuri tukipata kuona makosa yetu kuliko kuyaona mazuri yetu.Kwa hivyo kumbuka katika fungu hili kwetu kwamba Kristo anaelewa udhaifu ulio katika Kanisa lake,hata kati kati ya huduma yetu Hodari.

Kanisa la Efeso lilijawa na kazi. “ Nayajua matendo yako,na taabu yako,na Subira yako,na kuvumilia kwa ajili ya jina langu,wala hukuchoka.” Efeso lilikuwa Kanisa lenye bidi kiasi kwamba liliendelea na juhudi kwa kuvumilia,na halikuchoka katika lengo lake takatifu.Laiti tungelikuwa kama hivyo katika makanisa yetu yote! Nimeona miradi mizuri ya maana ikianzishwa na kuiachwa kuzimia kama moshi.Nimesikia mipango mizuri yenye matumaini yenye ilianzwa na kuiachwa.Kuvumilia kwa njia ya utakatifu ndiyo dhamana isiyoharibika.Katika miaka thelathini na mitatu ,twashukuru Mungu kwamba tumemfanyie kazi

bila kuchoka.Kumekuwa na kujaribu kila kitu,lakini hatujarudi nyuma. " Hii ndiyo kazi,hii ndiyo ajira," ili tushikilie hadi mwisho.Tumekuwa na hofu kiasi cha kwamba tungekatiza kazi yetu takatifu au kukomesha juhudi zetu takatifu! Hata hivyo Mungu ametusaidia.Kupitia kwa watu na njia,ukarimu na juhudi,ametusaidia.Kwa hiyo Malaika wa kanisa hawajakuwa tu Malaika wa mbinguni bali ni Malaika ambao ni binadamu; kwa sababu kwa udhaifu wa mwili na uzito wa roho nimefuata wito wangu.Kwa usaidizi wa Mungu bado natenda hadi leo, na kanisa hili kwa nyayo zake liko kwa upande wangu;ambayo sifa zote zi kwa Bwana,ambaye hachoki wala hazimii.Ambaye baada ya kuweka mikono yangu kwenye mpini,sijaangalia nyuma, lakini nimeangalia mbele,nikitengeneza mitaro; lakini imekuwa kwa neema ya Bwana peke yake.

Lakini Kanisa hili la Efeso halikuwa tu na bidi peke yake,bali lilikuwa na Subira katika mateso makali. Ananena kulihusu: "Nayajua matendo yako,na subira yako,na kuvumilia,wala hukuchoka." Mateso baada ya mateso yanawatembelea waaminifu, lakini wanavumilia kwa ujasiri na kwa bidii,na wanaendelea kumtaja Bwana wao.Hili lilikuwa jambo jema na Bwana alihidhinisha kazi yao; lakini bado kwa undani aliona ishara ya kurudi nyuma; walikuwa wameuacha upendo wao wa kwanza. Kwa hiyo kuna uwezekano wa Subira na uvumilivu na ujaziri ambao unafaa uwe,lakini kama vile tufaha iliyo na mdudu ndani yake,basi linaweza kuwa na kanisa wakati linaonekana mzuri kwa macho ya marafiki.

Kwa hivyo,uovu huu ulikuwa mbaya sana; ulikuwa upendo uliokuwa ukipoa: "Umeuacha upendo wako wa kwanza." " Hili si ni jambo la ajabu sana?" akanena.Hili ni uovu ulio mbaya sana kwa maovu yote; kwa sababu kanisa ndilo Bi harusi wa Kristo,na kwa Bi harusi kukosa kuwa na upendo ni kuanguka kwa mambo yote.Ni bure sana ikiwa mwanamke atasema amemtii na kila kitu ikiwa upendo kwa mume wake umepoa,kwa sababu jukumu lake kama mwanamke halitakamilishwa,amepoteza uhai na roho ya hali ya ndoa.Kwa hivyo wapendwa,hili ni suala letu la ajabu,upendo wetu kwa Kristo,kwa sababu linagusa moyo wa ushirika naye ambao ni taji na madhumuni ya Maisha ya kiroho.Kama Kanisa,ni lazima tumpende Yesu,la sivyo tumeipoteza sababu ya kuwepo kwetu.Kanisa halina sababu ya kuwa kanisa ikiwa halina upendo ndani ya moyo wake,ama kama upendo huo unapoa.

Je,sijawahi kuwakumbusha kwamba kila ugonjwa unaweza kutibiwa ila tu ugonjwa wa moyo? Lakini ikiwa ugonjwa wetu ni ugonjwa wa moyo,basi ni ugonjwa uliojawa na hatari nyingi; na ilikuwa hivyo katika harakati hii, " umeuacha upendo wako wa kwanza." Ni ugonjwa wa moyo,ungonjwa unaoua,ila tu Tabibu mkuu atakapoingia kati na kuukomesha na kuendeleza kazi yake.ndiyo katika mtu ye yote,kwa mwanamke yeyote na mwana wa Mungu,tukiacha hata kanisa kwa jumla,ikiwa upendo wa kwanza umeachwa,litakuwa jambo la hatari sana! Bwana turehemu.Kristo turehemu.Hili ndilo ombi letu mara moja.Hakuna kicho kilicho kuu kama hicho.Ukikosa upendo,umekosa yote.Tuuachie upendo wetu wa kwanza, tumeacha nguvu,na amani,na furaha na Faraja,na utakatifu.Niligundua kwamba Yesu alipata jambo hili kwa uchungu mkubwa.Sitaki nimletee huzuni mkubwa kama Bwana wa Kanisa badala ya kuangalia uso wake na kusema, "Nimeuacha upendo wangu wa kwanza." Ni nini unaweza kumpa ila upendo? Je,Kanisa linaweza kumnyima huu upendo?Kilicho kibaya ni kwamba Kristo alimwoa akiwa maskini akiomba,na ikiwa hatampa upendo, basi hatampa nini? Akianza kukosa uaminifu moyoni mwake,basi atakuwa na faida gani? Kwa nini,kwa sababu mwanamke yeyote asiye na upendo msumbufu na aibu kwa mumewe.Je,wapendwa itakuwa kwetu sisi pia? Je,tutamhuzunisha Emanueli? Je ,utakuwa hivyo? Kanisa la Mungu litamhuzunisha mbalo kwa

ajili yake aliraruliwa kwa ukombozi wake? Ndugu,dada,je Yesu anaweza kupata kwamba upendo wetu unaondoka,kwamba tunazimia kwa juhudi zetu kwa ajili ya jina lake? Je,twaweza kumhuzunisha hivyo? Je hiyo si ni kumsulubisha mara nyingine tena? Je,si anaweza kuishika mikono na kusema asubuhi ya leo kwamba, “ Hiki ndicho kidonda nilichopata kwa nyumba ya marafiki zangu.Ilikuwa ni bure kwa kuwafia,lakini bada ya kuwafia,wamekosa kunipa mioyo yao?”

Yesu haugui sana kwa dhambi zetu kama vile anavyougua kwa uvuguvugu wetu.Itakuwa jambo baya kwa moyo wangu; na pia natumai kwamba litakuwa jambo la kuhuzunisha kwa wote wanahusika,kwamba Bwana wetu atakuwa wa kwanza kugundua upoaji wa upendo wetu.Mwokozi alilenga ukosaji wa upendo; na alipousema,aliutaja kwa jina la kuomboleza. “Basi,kumbuka ni wapi ulikoanguka.” Anauita kuanguka kwa kuacha upendo wetu wa kwanza.Ndugu zangu,dada zangu,kanisa hili halijasajiliwa,halijaenda kando kwa kuyafuata mafundisho mapotofu,halijakuwa na uzembe, halijakuwa na uwoga wakati wa mateso; lakini dhambi hii moja ilijumuisha kila kitu kwamba halikupenda Kristo kama vile lilikuwa likimpenda, na Yesu anasema alianguka. Kuanguka kweli kwa sababu, “Ningedhani, “ ananena, “ kwamba ikiwa mshirika mmoja wa kanisa amelewa basi hiyo ni kuanguka.” Hiyo ni kuanguka kubaya, lakini ni kuaguka ikiwa tumelewa na ulimwengu,na kupoteza dhamani yetu kwa Yesu.Ni kuanguka kutoka kwa hali ya ushirika wa juu hadi kwa mavumbi ya ulimwengu.

“Umeanguka.” Neno hili laonekana kali sana masikioni mwangu hapana,siyo kali,kwa sababu upendo wake unautaja kwa njia ya kusikitisha; lakini linanguruma ndani ya roho yangu.Siwezi kulibeba.Ni ukweli wa kuhuzunisha. “ Wewe umeanguka.” Kumbuka ukikoanguka.” Kwa kweli,ewe Bwana, tumeanguka wakati tuliuacha upendo wetu wa kwanza kwako. Kiasi kikubwa ambacho Bwana wetu anaelewa.Roho Mtakatifu,tubarikie hayo! Neno la kwanza ni Kumbuka. “Umeuacha upendo wa kwanza.” Kumbuka basi ni nini upendo wa kwanza, na ulinganisha na hali ya sasa vile ilivyo.Awali,hakuna kitu kilichokuzuia kwa Bwana.Alikuwa uhai wako,upendo wako,furaha yako.Sasa hivi unaangalia kuburudika kwingine,kwa vitu vingine na mapambo yanayoshawishi moyo wako.Je,hujaaibika kwa jili ya haya? Awali hungechoka kwa kusikia kutoka kwake na kumtumikia.Haukuwahi kuchoka na Kristo na injili yake: mahubiri mengi,mikutano mingi ya maombi, kusoma kwingi kwa Biblia,hata kama ilikuwa mingi.Siku hizi mahubiri ni marefu,na huduma zimekosa maana kwako,na wewe umekuwa na hamu uliondoka kwa na upya wako.Hii inakuwaje? Wakati haukufurahishwa na Yesu kwa lo lote alilokufanyia.Ikiwa ulikuwa mgonjwa,au maskini,au ukitaka kufa,bado ungezidi kumpenda na kulibariki jina lake kwa vitu vyote.Anakumbuka uzoefu huo na anasikitika kwa kuodoka kwa uzoefu huo.

Anakwambia hivi leo hii, “ Nakukumbuka, hisani ya ujana wako, upendo wa wakati wa uposo wako; Jinsi ulivyonifuata huko jangwani, katika nchi isiyopandwa mbegu.” (Yer.2:2) Wewe ungemwendea Bwana kila mahali siku hizo; kupitia baharini,au kupitia motoni,ungemfuata;hakuna chochote kilichokuwa moto au mzito kwako wakato huo.Na wakati huu je? Kumbuka,kumbuka mahali ulikoanguka.Kumbuka nyapo,machozi,mazungumzo,unyakuzi wa siku hizo,kumbuka na ulinganishe na hali yako ya sasa.Neno litakalolifuata ni , “ Tubu.” Tubu kama vile ulivyofanya awali.Neno linalowahusu wenye dhambi linakuhusu wewe pia,kwa sababu umekosa sana.Omba msamaha kwa dhambi ambayo umefanya kwa kuacha upendo wake wa kwanza kwake.Uliishi kwa Maisha ya

utauwa,ukipumua upendo wake,ukiishi kwa ajili yake,basi hujafanya jambo lolote,lakini umeuacha upendo wako wa kwanza,je wajua kosa kubwa umelifanya kwa kuuacha upendo huo wa kwanza! Huo upendo ulistahili sana,sio? Kwa nini sasa umeuacha? Je Yesu amekosa kuwa na maan jinsi alivyokuwa? Je,sasa hukependi jinsi alivyokupenda? Sasa unaweza ukaishi bila yeye? Je,sasa kuna tumaini la wokovu bila yeye? Nakuagiza,utubu kwa yule ambaye alikupenda na upendo mkuu.Unapasw kumpenda kuliko vile ulivyompenda hapo mwanzo! Ewe moyo wangu hauna ukweli kama vile ulivyokuwa hapo awali? Ni jinsi gani moyo wangu umetenda maovu! Ni jinsi ganmi nina moyo usio na shukrani! Tubu! Tubu! Tubu! Tubu!

Kwa akili yangu,nikikumbuka fungu hili,wito wa kutubu unakua kwa sauti sana,kwa sababu ya kulitaja mara nyingi.Huyu ni Mwokozi Mtukufu akija kwa kanisa lake akiongea na Malaika wake kwa sauti nyororo ya utu wema.Anapanga kuwatembelea watu wake kwa utukufu wake wote na mamlaka,asipotarajia chochote ila tu kujitokeza kwa upendo kwa wateule wake kwa njia ambayo hajawahi kuufanyia ulimwengu.Na anaguzwa kwa kusema, “ Lakini nina neno juu yako,ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza.” Huu ni upendo-matembezi yaliyo na shutuma unaofaa shutumu. Ni dhambi gani iliyotendwa! Ni jambo la kusikitisha sana kwamba wakati Yesu anawajia Bi harusi wake anaongea akiwa na huzuni,na siyo furaha.Je,lazima ushirika mtakatifu,ambao ni divai ya mbinguni,unachukuliwa na sauti hodari ya lawama?

Naona chemchemiya juu ya ushirika wa karibu,ambayo maji ya uzima unatiririka kutoka kwa kianzo cha moyo wa Mungu.Je,mikondo hii si safi nay a dhamani? Ikiwa mtu atakunywa kutoka chemchemi hizi ataishi milele.Je,itakuwa kwamba hata katika vianzo vya vijito vitaporomoshwa na uchungu? Hata kama Kristo anatuongelesha,je,lazima aseme, “ Nina neno juu yenu?” Vunja moyo wangu,ili iwe hivyo! Basi tutubu kwa toba ya ndani wakati ladha yetu tulioichagua na mboga ya masikitiko,ili kwamba Mpendwa wetu wa dhati awe na kitu dhidi yetu.Twapaswa kuzirudia kazi zetu za kwanza mara moja.Watu wengi wanamjia Kristo wakiruka; na nimeona kwamba wengi ambao wanamjia mara nyingi wanafanya hivyo wakikimbia.Kufufuka kwa taratibu wa upendo wa mtu ni jambo ambalo wakati mwingine haliwezekani; kama vile kutarajia wafu wafufuke kwa kiwango.Upendo kwa Kristo ni upendo wa kuona,tunamwona,na tunashindwa nao.Tukipoa,jambo la muhimu la kufanya ni kumtazama hadi tulie, “ Nimezimia nafsi yangu aliponena.” (Wimbo 5:6).Ni wakati wa furaha sana ikiwa naweza kulia, “Kabla sijajua,roho yangu ilinileta Katikati ya magari ya wakuu wangu (Wimbo 6:12).Je ni furaha iliyoje Mungu akiturudisha tena mara moja mahali pale kwa wakati huu!

Ombi langu ni kwamba iwe hivyo asubuhi ya leo kwa yule ambaye anarudi nyuma.Jaribu kutubu siyo kwamba uwe na hisia za zamani, walakini ili ufanye kazi za kwanza,na uwe na jitahada,na juhusi,na utu wema,na kuwa mwombaji,kama vile ulivyokuwa! Tukikuona unapasua chupa,basi tutajua kwamba upendo wako wa zamani umerudi.Mwokozi wetu atusaidie kufanya vizuri Zaidi,ndiyo,bora kuliko vile tulivyofanya!

Basi nimekwambia jinsi Kristo aliyoweka,na nahitaji dakika chavhe kwa sehemu hii ya mwisho,kwa sababu nataka kuongea kwa njia ya dhati sana.Sina tamanio la kusema neno ili nionekana kuwa ndugu wa kweli anayewasihi kwa huruma ya ndani,kwa sababu kwa maovu yote ambayo nayakemea,naomboleza pia upande wangu.Tubariki,ewe Roho wa Bwana! Kwanza, anatushawishi kwa njia ya onyo: “ Nitakuja kwenu,” hivi upesi” ambayo halipo kwa

tafsiri ya awali: Tafsiri ya sasa imeliacha neno hilo.Bwana wetu huenda polepole kwa kazi ya kuhukumu: “Naja kwako,nami nitakiondoa kinara katika mahali pake,usipotubu.”

Hiyo lazima atafanya:hawezi kuruhusu mwanga wake uwe bila upendo,na ikiwa upendo wa kwanza umeachwa,kanisa linabaki kwa giza.Ukweli lazima ung’ae,lakini siyo mahali moja.Mahali hjapo lazima patengenezwe na upendo,la sivyo nuru hiyo itaondolewa.Lakini kinara pia kinawakilisha umuhimu: ndicho kinafanya kanisa ling’ae.Kazi ya kanisa ni kuhifadhi ukweli,ili uangaze majirani,ili uangaze ulimwengu.Mungu anaweza kukatishwa dhamana yetu, na atafanya ikiwa tutakatisha upendo wetu.Ikiwa Bwana wetu atatuacha,tutaendelea mbele na kazi zetu kama vile tulikuwa tukifanya,lakini hakuna matokeo tutakayoyapata: Tutaendelea mbele na shule ya kufundisha Watoto siku ya kuabudu,makao yetu,makanisa yaliyo chini yetu,lakini hatukamilishi jambo lolote.Wapendwa,twaweza kuendelea mbele kituo cha mayatima,Chuo cha kujifunza,Kuuza vitabu,Jamii ya Kufanya Uinjilisti,Kuwapa watu vitabu,na yote hayo,lakini hakuna jambo lolote litafanyika ikiwa mkono wa Bwana hautakuwa wazi kwetu.Je,nitawashawishije,japo kwa maneno ya onyo la Mkombozi wetu? Mpendwa,nakusihi toka kwa roho ili usimenyane na hatari hizi,ili usikimbie hatari hizi; kwa sababu hautatarajia kuliona kanisa au wewe mwenyewe kuachwa bila nuru ya Mungu, na kukaa gizani, inabidi ukae ndani ya Kristo,na uzidi kumpenda Zaidi na Zaidi.

.Kumbuka kwamba,wale wanaopoteza upendo wao wa kwanza wanatangatanga,wanamwacha Mungu. “Lakini,” Anena Bwana, “ ikiwa utatunza upendo wako wa kwanza hautatangatanga,lakini utakuwa na ushirika wa karibu.Nitakuleta karibu katikati.Nitakuleta ule matunda ya mti wa uzima ulio katikati ya paradiso tukikaa katika pendo lake.Je,ni furaha iliyoje! Ni thawabu kubwa iliyoje tunayopata kutoka kwa upendo! Mbingu iliyo duniani ni upendo kwa Yesu.Hili ndilo la kwanza na la mwisho kwake tukifurahi kwa upendo ambao ndio mwanzo na mwisho. Kumpenda Kristo ni njia nyingine ya kusema Paradiso.Bwana,nifanye nijue jambo hili kwa uzoefu wa kila siku. “ Unaruka juu juu ,” analia.Ndiyo,naimiliki.Ee laiti ningekushawishi ili uruke kwa mbawa za upendo wa kibingu! Kuna uchungu kwa upendo unaopoa:unakula roho zetu,na unatufanya dhaifu,na kukosa nguvu,na kupungua.Lakini upendo wa kweli ni Zaidi ya utukufu.Tazama urefu,kina kinachong’aa,kina cha utukufu,milima ya milele ambayo Bwana wa uzima atawaongoza wale walio waaminifu kwake kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu kwa kutuleta karibu na Bwana Harusi war oho zetu.Amina.

SEHEMU ZA MAFUNGU LITAKALOSOMWA KABLA YA MAHUBIRI HAYA **Ufunuo 1:0** ; **Ufunuo 2:1-7** .